

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

Wahusika

Angela

Annie

Djamila

Anita

Pinto

Tom

Vijana wawili wenye umri wa miaka 17 na 18

Utangulizi

Karibu katika kipindi cha sikiliza ujifunze kwenye sehemu nyingine ya mchezo Malaika wa kila mtu, mchezo ambao unayaangazia maisha ya vijana wanne ambao ni marafiki.

Katika kisa cha leo, Djamila bado anabughudhiwa na mjombawe Imrat na Tom angali kwenye shinikizo ya marafiki za kumtaka ajionyeshe kama kweli yeye ni bingwa wa kutongoza wasichana.

Angela naye kapata uja uzito baada ya kulala na mpenzi wake kwa mara ya kwanza mpenzi ambaye hawakujuana kwa muda mrefu, na juu ya hilo ameambukizwa virusi vya HIV. Na sasa anajiandaa kuondoka kwa wazazi wake na pia kuwaaga rafiki zake Djamila na Annie ili kuanza maisha mapya kwengine.

Je nini kitatokea katika kisa cha saba cha mchezo huu, Malaika wa kila mtu, tega sikio.

SURA YA KWANZA: KWENYE BUSTANI

SFX MJINI, MCHANA, SAUTI ZA MAGARI

ANNIE Yaani siamini Angela mamako anakufukuza kinyama namna hii.

ANGELA Sio vibaya sana, Annie, ngoja utaona, nipe muda tu, Pinto kanambia ameshajiweka tayari kuendelea na maisha. Na unajua kliniki ya mjini iko karibu tu na anapoishi.

ANNIE Alaa! Basi hata mimi huenda kwenye kliniki hiyo hiyo kwa matibabu. Wajua kwa nini, kwa sababu hakuna mtu atakayenitambua! (kicheko) Ntakupigia simu basi kwanza, halafu tukutane, sawa?

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

ANGELA Sawa kabisaa! Angalia Djamila wewe unafikiriaje?
DJAMILA Ennnh... je ikiwa haitafanikiwa, Angie namaanisha mpango wako na Pinto? Unajua nyinyi wenyewe hata hamfahamiani. Je, ikiwa hamtapendana.
ANGELA Ah ikiwa basi mambo hayatakwenda sawa, mjomba wangu Billy ameniahidi kwamba ninaweza kwenda kuishi kwake pamoja na Layla na Mo.
DJAMILA Kwa hiyo unachosema ni kwamba utakuwa na familia huko, basi ni vizuri, nafurahi kusikia kama una watu wa kukushika mkono. (kwa huzuni)
ANGELA Anaenitia wasiwasi ni mamangu Djamila, amekazia moyo kweli kweli, utadhani kitu gani sijui hebu fikiria hata nduguze hazungumzi nae. Anafikiri kila mmoja ni adui yake.
DJAMILA Pengine unamkumbusha mbali enzi za ujana wake, nani anayejua? Ulinambia humjui babako na wala mamako hajawahi kuolewa. Pengine stori yako inafanana na kilichomkuta ujanani, labda kuna kitu kilichompa dhiki sana na sasa maisha yako yanamkumbusha alikotoka?
ANNIE (Anacheka) ooooh Djamila, si ajabu umekuwa ukihudhuria mafunzo juu ya asilia ya maisha.
DJAMILA Napenda sana, kwanza yananifumbua macho kujua asilia yangu binfasi juu ya tabia yangu, kwa nini nina haya nyingi au kwa nini nalialia kuhusu mambo fulani fulani.
ANGELA Ni kweli tunachokisoma tunajisomea sisi wenyewe kuhusu maisha yetu. Annie? Mimi lakini nna wasiwasi na wewe.
ANNIE Najua nimekuwa rahisi mno kudanganyika. Nataka mambo mazuri katika maisha. Lakini mambo hayaendi vile nnavyotaka mimi (kimya kidogo) Lakini hili sio kuhusu mimi, ni juu yako, unakwenda kuanza maisha mapya.
ANGELA Nikumbatie basi, na tutaonana hivi karibuni...
ANGELA Na wewe Djamila, usiwe bubu umesikia, sema kinachokukera na ukatae, mwambie huyo mjombako aache kukuchezea chezea.
SFX MUZIKI WA KUFUNGA

SURA YA PILI: MASHAMBANI, BARABARANI

SFX SAUTI ZA NDEGE NA WATU WAKITEMBEA
ANITA Paleeee ndo mjomba Billy anakoishi, sasa tumepita

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

nyumba 15, nafikiri tumefika, ni hapa... hebu bisha wewe Angela.

SFX ANAGONGA MLANGO WA MBAO. UNAFUNGULIWA

PINTO Bi Selebi, habari ya saa hizi.

ANITA Pinto Maithibe, umelitia doa jina la familia yangu.

PINTO Ndio Bi Selebi.

ANITA Sasa utabeba jukumu lako na umchukue huyu binti.

PINTO Hakuna wasiwasi, bi Selebi, na samahani sana.

ANITA Ni hayo tu yalonileta hapa, sina kingine cha kusema.

PINTO Huingii ndani basi bi Selebi?

ANITA La hasha, nakwenda kwangu moja kwa moja, tutaonana tena wakati mtakapokuwa mmeoana na kuwa wacha Mungu. Kwa heri, Angela.

ANGELA Nisamehe Ma. Kwa heri.

SFX Sauti za watu wakitembea zinatokomea.

PINTO Lete begi nikusaidie... Ingia ndani.

SFX MLANGO UNAFUNGWA, SEBULENI

PINTO Hii ni kama ndoto.

ANGELA Sio ya kutisha?

PINTO Hapana Angela... nina kumbukumbu za furaha tu juu ya tuliyoyafanya usiku ule.

ANGELA Sasa kama ni hivyo mbona hukunipigia tena simu tangu wakati ule?

PINTO Ni kweli, lakini nilifikiri kwamba unakaa mbali sana na isitoshe bado uko shule. Kwa hiyo niliona haingekuwa sawa kukutafuta.

ANGELA Basi sasa sirudi tena shule, siwezi kuendelea na masomo.

PINTO Najua. Samahani sana kwa yote haya. Lakini kwa nini hukunipigia simu kunieleza kama una mimba?

ANGELA (Acheka kidogo) mie mwenyewe sikujua...

SFX MLANGO WAFUNGULIWA

PINTO Unaweza kulala chumba hiki, na begi lako naliweka humuhumu ndani, wewe jisikie umefika, uko nyumbani hapa. (Anakohoa kohoa)

ANGELA Uko sawa lakini?

PINTO Ni kikohozi tu. Wiki sasa nnacho lakini kitakwisha hivi karibuni. Twende tukatengeze chai (kikohozi kinatokomea)

SURA YA TATU: KWENYE KELELE

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

SFX WAVULANA WAKIJISIFIA KUHUSU WASICHANA
AMBAO WAMESHAWABUSU NA KULALA NAO

MV. WA KWANZA Vipi Tom, mshikaji? Naona Annie alikudharau kweli
siku ile kwenye basi, na kukuona mtoto.

MV. WA PILI Na wajua tena rafiki yangu Tom kwamba ukubwa wa mtu ni
muhimu!

SFX KICHEKO CHA UCHOKOZI
TOM Kwa mimi muhimu ni ubora wa kitu sio kiwango cha kitu
mmesikia

WAV. WOTE Ok Tom, endelea kusema hivyo!
WA PILI Wewe Tom ni mdogo sana kwa yule binti tena pia huna
mwili.

SFX VICHEKO
TOM Ha Ha Ha! Sihitaji kuwa na mwili, niko sawa mimi.
WA KWANZA Nakuhakikishia Tom huwezi kumpata yule binti.
Tuwekeane.

TOM Kiasi gani tuwekeane?
WA KWANZA (akicheka) Siwekeani mimi lakini ukimpata nitakununulia
bia moja!

SFX WAVULANA WAKIMCHOKOZA
TOM Changamoto gani hii! Sawa nakubali.
WA PILI Mpigie simu basi kama unayo namba yake!
WA KWANZA Awe na nambari ya Annie ya nini huyo?
TOM Namba ninayo hii hapa, mtazame kichwa kama yai... ngoja
niipige

SFX MLIO WA SIMU
TOM Hallo? nazungumza na Annie?
ANNIE (kwenye simu) Nani huyu?
SFX WAVULANA WANONG'ONEZANA
TOM Ni mimi Tom hapa wajua nimeweka ahadi juu ya yale
tuliozungumza mara ya mwisho, si wajua
Oh kwani umekuwa mlinzi wangu...

ANNIE Ikiwa utanihitaji ndio ningependa kukuona Annie.
TOM Unafanya hivi kwa sababu uko na rafiki zako hapo sio?
ANNIE Eti ?
TOM Nawasikia huko nyuma nyuma wakizungumza au unafikiri
sina masikio.

TOM (kwa hasira) Ok, sahai basi...
ANNIE Hapana sikiliza Tom, aaah angalia, sasa hivi mamangu
hayupo, njoo basi ukitaka.

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

TOM (kwa furaha) Sawa nisubiri dakika kumi nitakuwa nimefika, poa, bye.
SFX WAKISHANGILIA
TOM (kwa raha) Yes!! Ntarudi kufuata bia jamaaa.
MUZIKI UNAMALIZIA

SURA YA NNE: NDANI

ANNIE Enhe nambie, sasa uko hapa ili upate cha kujisifia kwa marafiki yako au vipi? Utatunga hadithi gani sasa ya kujisifia baadae.

TOM Sikiliza Annie najua ni upuuzi. Lakini nyinyi wasichana pia mnafanya hivyo hivyo. Nishawahi kuwasikia mkichokozana kuhusu wanaume. Mtu ambaye hana tabia hiyo ni Djamila.

ANNIE Haya sawa, na ngoma unayoipiga siichezi mimi...

TOM Sikiliza nitakwenda sasa hivi nikawaambie nimebadili mawazo yangu. Siogopi bwana kuwaambia.

ANNIE Ah tuendelee tu kuongea kwa kuwa tayari uko hapa, unaonekana unataka kujua mengi kunihusu na wale nnaotembea nao.

TOM Wewe ni mrembo Annie, unavutia, naona unajiaibisha sana unapotembea na watu kama SPIKE au yule jamaa mzee kweli. Kwanza vipi mkono wako?

ANNIE Nimepata nafuu, nasikitika uliona tukio lile

TOM Mimi pia nasikitika kwa sababu sio vizuri kuona msichana akipigwa namna ile.

ANNIE Yaani wewe mzuri kweli. Kwa hiyo unaona afadhali nikukubali wewe?

TOM Sio siri, na bila ya kuficha ningependa uwe wangu. (akimsogelea karibu) naomba nitoke out na wewe japo mara moja ili upate kunijua, nami nikujue, tufanye ni out ya majaribio. Wasemaje?

ANNIE (akicheka taratibu) Nina mpenzi, Tom.

TOM Yule Spike mwendesha taxi sio? au ni Jet anayeendesha gari la kifahari?

ANNIE (Kwa kejeli) Hmmm sasa kwanini unataka kuwa namba tatu?

TOM Unatumia Mpira lakini?

ANNIE (Ashtuka) Nini?

TOM (Aghadhabika) Ni swali rahisi tu. Ikiwa unatembea na

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

wanaume wawili - au pengine hata ni watatu - kwa wakati mmoja, je unatumia mpira wa Condom?

ANNIE Sikiliza, Tom, hakuna hata mwanamme mmoja anayetaka kutumia condom. Na wewe?

TOM Silali na wanawake ovyo ovyo. Lakini ningekuwa nafanya hivyo, ningetumia Condom. kwa hivyo hutumii kinga yoyote, sasa kwa nini nihatarishe maisha yangu kupata magonjwa ya zinaa kwa sababu tu ya kulala na wewe?

ANNIE (Ashtuka) Tom sasa hivi ulikuwa ukisema unataka niwe mpenzi wako...

TOM Ndio lakini sikutaka niwe mimi na wenzangu

ANNIE Nina miaka 16 Tom, wewe unafikiria nini unaponizungumzia hivyo ennhe? unafikiri ntakuwa mkeo? Tia akili...

TOM Wewe tia akili Annie. unafikiri Spike au huyo Jet wako hawana wapenzi wengine? Pengine uko nambari tatu katika orodha zao! je unajua kama maradhi ya zinaa na HIV yanaambukiza? Tena kama moto wa mwituni... unajua haya yote... sijui kwa nini nakueleza na wewe ni bingwa mzoefu katika mambo hayo... lakini unachofanya ni kufumbia macho.

ANNIE (Kwa hasira) Yote yajia wapi? Nafikiri afadhali uondoke Tom. Umevuka mpaka. Halafu waambie marafiki zako kwamba tumelala pamoja na umepata ugonjwa wa zinaa, wasikia, nenda kawaambie! (afunga mlango kwa hasira)

ANNIE (Alia kwa uchungu) Hana adabu, anawezaje kunambia maneno yale!

SFX SIMU INALIA

ANGELA Vipi swahiba, nilitaka kukujulisha tu kwamba nitakwenda kliniki jumanne ijayo asubuhi, maanake ulisema tunaweza kukutana, waonaje? Jumanne kwako itakuwa sawa? (kimya) Annie vipi, uko? Lakini mbona umenyamaza mwenzio nakuuliza.

ANNIE (Kwikwi... anapasua kilio) Angela nina shida kubwa mwenzio! wewe ulikuwa huna ujalo maskini ukaambukizwa maradhi siku yako ya kwanza ulolala na mpenzi wako. Na mimi narandaranda na kila mtu bila ya kutumia kinga! Nimekosa haya Angela, sio sawa kabisa nasikia vibaya sana, sio haki!

Kila mtu ana malaika (07) - Msichana mjamzito afukuzwa nyumbani

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

HITIMISHO

"Malaika wa kila mtu" ni mchezo uliotungwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu mwasimba. Hadi hapo kwa leo ndio tumefika mwisho katika kipindi cha sikiliza ujifunze.

Katika kisa kingine cha mchezo Malaika wa kila mtu, Pinto anazidiwa na kikohozi, Jet nae hali yake inazidi kuwa mbaya baada ya kupata vipepele katika sehemu zake za siri, wakati Angela anajifunza mengi kila uchao kuhusu virusi vya HIV alivyoambukizwa na anazidi kujiamini.

Kumbuka, ukiwa unataka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine au unataka kuwaambia marafiki kuhusu mchezo huu, tafadhali tembelea tovuti yetu kupitia anuani ya www.dw.de/lbe.

KWA HERI.